

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

(Mawasiliano yote yafanywe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

MKOA: NJOMBE

Simu: +255 - 26 2790120
Nukushi: +255 - 26 2790128
Barua pepe: ded@ludewadc.go.tz
Tovuti: www.ludewadc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 19,
Ludewa,

TAREHE: 10 Augusti, 2017

TANGAZO

TANGAZO

TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA LUDEWA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KODI YA MAJENGO SURA YA 289 NA MAREKEBISHO YAKE YA MWAKA 2015 PAMOJA NA SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA SURA YA 290 NA SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA ZA MWAKA 2016 UMEANZA RASMI AMBAPO KILA MMILIKI WA JENGO ANATAKIWA KULIPA KODI YA JENGO KWA MUJIBU WA VIWANGO VILIVYOPITISHWA NA HALMASHAURI KWA UTHAMINI WA MKUPUO.

JEDWALI LA TOZO ZA KODI YA MAJENGO ZINAPATIKANA KATIKA MBAO ZA MATANGAZO MAENEO YAFUATAYO: BOMANI, OFISI YA KATA LUDEWA, OFISI YA KATA MLANGALI, OFISI YA KATA LUGARAWA, OFISI YA KATA MANDA NA KATIKA TOVUTI YA HALMASHAURI YA WILAYA LUDEWA (www.ludewadc.go.tz).

MALIPO YOTE YAFANYIKE KUPITIA OFISI YA MTENDAJI WA KATA KWA WOTE WALIO MBALI NA OFISI ZA HALMASHAURI NA WALIO JIRANI NA HALMASHAURI WAFIKE OFISI YA AFISA BIASHARA ILIYOPO NDANI YA JENGO LA HALMASHAURI (BOMANI). MALIPO YOTE YAFANYIKE NDANI YA MWEZI WA NANE 2017 (AUGUSTI, 2017) ILI KUEPUKA KULIPA FAINI PAMOJA NA HATUA NYINGINE ZA KISHERIA.


TAFADHALI PITIA JEDWALI HILI ILI UWEZE KULIPA KODI YA JENGO KADRI INAVYOSTAHILI:

**JEDWALI LA VIWANGO VYA UTOZAJI KODI ZA MAJENGO WILAYANI LUDEWA
KWA MWAKA**

SN	AINA YA JENGO	MAENEO YALIYOPIMWA (TSHS)	MAENEO YASIYOPIMWA (TSHS)
1	Majengo ya makazi ya kawaida Kata ya Ludewa	10,000.00	5,000.00
2	Majengo ya makazi ya kawaida nje ya Kata ya Ludewa	5,000.00	3,000.00
3	Majengo ya ghorofa (kiwango kwa ghorofa moja)	40,000.00	20,000.00
4	Majengo ya Makazi na Biashara Kata ya Ludewa	20,000.00	15,000.00
5	Majengo ya Makazi na Biashara nje ya Kata ya Ludewa	15,000.00	10,000.00
6	Majengo ya Biashara Kata ya Ludewa	30,000.00	20,000.00
7	Majengo ya Biashara nje ya Kata ya Ludewa	20,000.00	15,000.00
8	Viwanda vidogo	100,000.00	50,000.00
9	Viwanda Vingine	500,000.00	300,000.00
10	Vituo vya mafuta (Shell) Kata ya Ludewa	1,000,000.00	600,000.00
11	Vituo vya mafuta (Shell) nje ya Kata ya Ludewa	800,000.00	500,000.00
12	Maghala ya Mafuta (Depot)	2,000,000.00	1,000,000.00
13	Maghala mengine Wilayani	500,000.00	300,000.00
14	Maghala mengine	300,000.00	200,000.00

NB: Majengo mengine ambayo hayajatajwa katika jedwali hapo juu yatatozwa kodi ya majengo kwa kiwango cha 0.2% ya thamani ya jengo baada ya kufanya uthamini kwa majengo ya biashara.

Imetolewa na:


 Gladness Mwanoo
 Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
 HALMASHAURI YA WILAYA
LUDEWA.
10/8/2017

Mkurugenzi Mtendaji
 Halmashauri ya Wilaya
 Ludewa